**TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**
**KISWAHILI**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**SEHEMU YA A: USHAIRI (SWALI LA LAZIMA)** (alama 20)

1. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1) Hadhira e pulikeni, kisa changu mpaeni,
Mpateni mweleweni, mchekeni, mlieni,
Funzo lake mpateni, uamuzi mfanyeni,
Kisa hiki asilani, sisahau maishani.

2) Cha nne niliingiya, mtoto kafurahiya,
Malkia ungedhaniya, duniani meingiya,
Mapambo lijipambiya, kung'ara kikang'ariya,
Kisa change chatokeya, mwanzowe nafunguliya.

3) Darasani lizembea, bidii sikutilia,
Starehe nakwambia, nilipenda najutia,
Kimadaha litembea, tausi nilitulia,
Kisa kilinigonjea, mtume! Ningalijua.

4) Muhula kutamatika, dafu sikufua, kaka,
Enda, Ewe, Embe, fika, alama duni, viraka,
Nilipokea waraka, mzazi kahitajika,
Kisa kijatambulika, nakuomba makinika.

5) Muhula wa pili sasa, nikarudia makosa,
Sikupigeni msasa, makali nikayakosa,
Kisu sikunoa hasa, sikukata cha darasa,
Kisa ndicho hicho sasa, ninakupa pasi pesa.

6) Sasa muhula wa tatu, umetimia wanetu,
Mtihani kama chatu, nimeuogopa, mtu,
Sijausomea katu, ningalilindaje utu?
Kisa mkasa wa chatu, kilinipata wa kwetu.

7) Mbwa katu hafi maji, kiona ufuko, maji,
Tajaribu sife maji, hata akiyanywa maji,
Ilibidi twende jiji, kuwasaka wajuaji,
Kisa change mfumbaji, sasa dawa lihitaji.

8) Mpango ulitolewa, mchango ulipangiwa,
Pesa tele litolewa, na simu kununuliwa,
Mtandao liwekewa, 'kunani' kupakuliwa,
Kisa cha simu kujuwa, linifanya kupagawa.

9) Tulikata dari ona, simu yetu kufichana,
Usiku tulikutana, maswali kurushiana,
Majibu tulipeana, 'panga' kabadilishana,
Kisa kinajulikana, vile nilivyokazana.

10) Niliyangoja majibu, nikiwa na hamu, babu,
Nilikimya kama bubu, nisije toa aibu,
Nilivichoma vitabu, bila kuwa na sababu.
Kisa kawa masaibu, kashindwa kuyaharibu.

11) Kutangazwa matokeo, nakumbuka hadi leo,
Lilishangaza toleo, sikuamini redio,
Lipokea matokea, yalinitia kimbio,
Kisa change mchocheo, haya yangu mapokeo.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

12) Nilifeli mtihani, sababu simu juweni,
Najuta nisameheni, nijilaumu moyoni,
Ningalijua mbeleni, ningalisoma jamani,
Kisa nimemalizeli, wenzangu mzindukeni.

13) Watahiniwa mlipo, msiwe mithili popo,
Skuli kwenu kuwepo, nia mpate malipo,
Bidii hapo mlipo, toa uzembe pasipo,
Kisa change kingalipo, simu daima siwepo!

**MASWALI**

a) Taja anwani mwafaka ya shairi hili. (alama 1)
b) Fafanua mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
c) Bainisha nafsi lengwa katika shairi hili. (alama 1)
d) Changanua arudhi zilizotumiwa na mtunzi wa shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa kumi katika lugha nathari. (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno na vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
g) Eleza maana ya maneno na vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
(i) Sikukata cha darasa
(ii) Yalinitia kimbio
(iii) Kupagawa

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Nashukuru sasa umeanza kuona mambo yanavyostahili kwenda."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa zozote **nne** za msemaji. (alama 4)
c) Fafanua maudhui ya ufisadi kama yalivyoangaziwa na mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 12)
3. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia – Mstahiki Meya. (alama 20)
a) Majazi
b) Taharuki

**SEHEMU C: RIWAYA**

***KIDAGAA KIMEMWOZEA* – *K. WALIBORA***

**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Kutowajibika kwa viongozi baada ya mkoloni kuondoka ni dhahiri." Jadili kauli hii kwa mujibu wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

5. "Hizi kurani zako ndizo zifanyazo nisije huku …"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika dondoo hili kwenye riwaya. (alama 6)
c) Eleza maisha ya msemaji yalivyokuwa kwa mujibu wa Riwaya ya Kidaa Kimemwozea. (alama 10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI.**

**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine - K. Walibora na S.A. Mohammed -.**

**Jibu swali la 6 au la 7**

***"Damu Nyeusi" (K. Walibora)***

6. "Nimemwita bwana huyu aje huku juu kusudi mumwone."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa **tatu** za mzungumzaji. (alama 6
c) Jadili maudhui ya ubaguzi namna yanavyojitokeza katika hadithi husika .(alama 10)

**au**

7. Kwa kurejelea hadithi zozote **tano** katika Diwani Damu Nyeusi, jadili namna ambavyo wahusika wa kike wamesawiriwa. (alama 20)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8.
a) (i) Eleza maana ya ushairi simulizi. (alama 2)
(ii) Eleza sifa **tano** za ushairi simulizi. (alama 5)
b) (i) Eleza maana ya ushairi simulizi. (alama 3)
(ii) Eleza sifa **nne** za matambiko. (alama 2)
Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479